**HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA MENEJIMENTI KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI TAREHE 13/12/2021**

**A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA: -**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndaki S. Mhuli | - Mkurugenzi Mtendaji | -Mwenyekiti |
| 2. Hidaya Yusuph | -Afisa Utumishi | - Katibu |
| 3. Iman Masebu | -Mwanasheria | - Mjumbe |
| 4. Muhidin H. Khalfan | -Afisa Kilimo | - Mjumbe |
| 5. Ally Omary | -Afisa Mipango | - Mjumbe |
| 6. Idda Brono | -Mratibu TASAF | - Mjumbe |
| 7. Imelda J. Hokororo | -Afisa Biashara | - Mjumbe |
| 8. Marton John | -Kaimu Afisa Elimu Sekondari | - Mjumbe |
| 9. Lameck G. Lugola | - Kaimu Mthibiti Ubora | - Mjumbe |
| 10. Dr. Godfrey Kayombo | - Afisa Mifugo | - Mjumbe |
| 11. Jobson R. Jobson | - Katibu TSC | - Mjumbe |
| 12. Dastan Kisaka | - Afisa Ardhi | - Mjumbe |
| 13. Stephen Mabuga | - Afisa Maendeleo ya Jamii | - Mjumbe |
| 14. Frank Lema | - Afisa Tehama | - Mjumbe |
| 15. Melkzedek B. Huruma | - Afisa Misitu | - Mjumbe |
| 16. Jonas Twimanye | - Afisa Mipango | - Mjumbe |
| 17. Abddilahi I. Mohamed | - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi | - Mjumbe |
| 18. Lynus Kagoma | - Afisa Manunuzi | - Mjumbe |
| 19. Joseph Mutahaba | - Afisa Elimu Msingi | - Mjumbe |
| 20. Dr. Joseph Malima | - Mganga Mkuu | - Mjumbe |
| 21. Itendele Maduhu | - Mweka Hazina | - Mjumbe |

**B.SEKRETARIETI**

| | |
|---|---|
| 1. Cosmas Makalla | - Afisa Habari |
| 2. Nusura Kabuli | - Katibu Muhtasi |
| 3. Fabius Jeremiah | - Afisa Utumishi |

**MUHT. NA.5/CMT/2021/2022/1.KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kufungua kikao saa 08:05 Mchana.

**MUHT.NA.5/CMT/2021/2022/2.KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zifuatazo zilithibitishwa:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kuidhinisha Muhtasari wa kikao cha Menejimenti wa tarehe 13 Oktoba, 2021
4. Yatokanayo

5. Kupitia Muhtasari wa kikao cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa tarehe 4 Novemba, 2021
6. Yatokanayo
7. Kupitia taarifa ya Mapato na Matumizi ya mwezi Oktoba, 2021
8. Kupitia taarifa ya Mapato na Matumizi ya mwezi Novemba, 2021
9. Ujenzi wa madarasa ya UVIKO - 19
10. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
    i. Machinjio kasanda
    ii. Vibanda soko kuu
    iii. Mnada wa mifugo kihomoka
    iv. Wakusanya mapato – mikataba mipya
11. Ujenzi wa Miradi inayotelekezwa kwa mapato ya ndani
12. Kufunga kikao

**MUHT.NA.5/CMT/2021/2022/3.KUIDHINISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI WA TAREHE 13 OKTOBA, 2021**

Muhtasari uliidhinishwa na kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**MUHT.NA.5/CMT/2021/22/4. YATOKANAYO**

- **Kuhusu changamoto zinazojitokeza kwenye kampuni.**

Afisa biashara aliwasilisha taarifa kisha wajumbe kutoa mapendekezo kama ifuatavyo;

i. Muundo ulioidhinishwa uzingatiwe- Idara na vitengo vizingatiwe
ii. Kutangaza na kufanya soko kuwa hai
iii. Kuboresha mawasiliano kata ya Kakonko na mkoa wa Cankuzo
    - Mawasiliano yamefanyika bado ufuatiliaji unaendelea
iv. Dira na Dhima
    - Meneja awe na mkakati na mpango kazi wa mwaka
v. Kuwa na ratiba maalum ya vikao.

- **Kuhusu muundo.**

Wajumbe walieleza kwa sasa ni vigumu kutekeleza muundo kama ulivyo kwani mapato bado yapo chini, hivyo maboresho yatafanyika baadaye baada ya mapato kupanda.

- **Kuhusu ajira mpya za watumishi**

Afisa Utumishi aweke mwendelezo wa hatua iliyofikiwa katika kushughulikia ajira mpya za watumishi. Afisa Utumishi alieleza Barua tayari zimeandaliwa kuomba ajira mpya na kumbukumbu namba zimewekwa.

- **Kuhusu mwalimu aliyempa mimba mwanafunzi katika shule ya msingi Nyamtukuza.**

Afisa Elimu Msingi afuatilie suala hili ili hatua za kinidhamu zichukuliwe na kufunguliwa mashtaka. Aidha taarifa iwasilishwe kikao kijacho.

- **Kuhusu hoja za ukaguzi za NAO.**

Hoja zimewasilishwa na Menejimenti imejadili kwa kina na kuwasilisha hoja kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Nje (CAG).

**MUHT. NA.5/CMT/2021/22/5. KUPITIA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA WA TAREHE 04 NOVEMBA, 2021**

Muhtasari ulipitiwa na Menejimenti na kuboreshwa.

**MUHT. NA.5/CMT/2021/22/6. YATOKANAYO**

- **Kuhusu bima ya afya.**

Mganga mkuu afanyie kazi suala hili.

**MUHT. NA.5/CMT/2021/22/7. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUANZIA MWEZI JULAI HADI NOVEMBA 2021.**

Mweka Hazina aliwasilisha taarifa kisha wajumbe kujadili kama ifuatavyo:-

- **Kuhusu ushuru wa pamba.**

Afisa Mapato alieleza ushuru umeanza kukusanywa, hivyo bado milioni 8 ambazo zinategemewa kulipwa Januari, 2022.

- **Kuhusu ushuru wa Kahawa.**

Ilielezwa hii inatakiwa kulipwa kutoka Kata ya Muhange hivyo ufuatiliaji unaendelea kufanyika.

- **Kuhusu ushuru wa Muhogo.**

Afisa Mapato alieleza ushuru huo unatarajiwa kukusanywa Januari, 2022

- **Kuhusu ushuru wa kupaki malori**

Mweka Hazina alieleza kwa sasa hawakuwa wanatoza ushuru huo kutokana na kukosa miundombinu eneo la kupaki magari hayo. Wajumbe waliazimia kuwa Mweka Hazina atafute kutafuta mgambo na kuwaweka eneo husika ili kutoza ushuru.

- **Kuhusu ushuru wa madini ya ujenzi.**

Mweka Hazina afuatilie kwani mapato ni kidogo. Mwenyekiti alisisitiza ufuatiliaji ufanyike kwani kwa sasa kuna ujenzi wa mradi wa madarasa kupitia fedha za UVIKO-19

- **Kuhusu ushuru wa mauzo ya viwanja.**

Afisa Ardhi afuatilie hilo.

- **Kuhusu mapato yatokanayo na Ukumbi wa Mikutano.**

Ilielezwa mapato ni 600,000/= tu. Mwenyekiti alisisitiza Idara ambazo zimetumia ukumbi zilipie mfano TASAF na Idara ya Kilimo. Aidha Mwenyekiti alitoa maelekezo kuwa ni marufuku kutumia ukumbi nje ya Halmashauri bila ruhusa yake.

- **Kuhusu ushuru wa upimaji wa nyama.**

Afisa Mifugo alielekezwa kufuatilia mapato ya upimaji nyama kwa mwezi Novemba, 2021, Kwani hakuna mapato yaliyoainishwa.

- **Kuhusu mihuri ya nyama.**

Mwenyekiti alihoji mihuri ya nyama kununuliwa imefikia wapi. Mwenyekiti alisisitiza suala hilo lifanyiwe kazi ili mihuri hiyo inunuliwe.

- **Kuhusu ushuru wa matangazo kuwa kidogo.**

Wajumbe walieleza kuwa matangazo yanafanyika lakini ushuru ni kidogo hivyo Afisa biashara afuatilie hilo.

- **Kuhusu ushuru wa Kahawa.**

Afisa kilimo alieleza ushuru huo unakusanywa kupitia mashine za POS. Aidha kwa mwezi Novemba 2021 hakuna ushuru uliokusanywa.

- **Kuhusu milioni 21 za UVIKO-19 zilizokuja nje ya bajeti.**

Wajumbe walishauri kipengele hicho kifanyiwe marekebisho.

- **Kuhusu fedha za ujenzi wa vyoo kupitia fedha za UVIKO- 19**

Mkurugenzi Mtendaji aliwaagiza Afisa Mipango na Afisa Elimu Msingi kuwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha hizo. Afisa Mipango alieleza shule tano (5) zimepokea fedha za UVIKO-19 kila moja **6,600,000/=** na shule 2 zimepokea fedha pia.

**Taarifa ilipokelewa.**

**MUHT.NA.5/CMT/2021/22/ 8. TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA YA UVIKO - 19.**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa kama ifuatavyo;

| **HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **NA** | **Jina la Mradi** | **Fedha zilizoidhinishwa** | **Mapokezi hadi 13/12/2021** | **Matumizi hadi 13/12/2021** | **Asilimia ya matumizi** | **Maelezo** |
| **1.0** | **MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19** | | | | | |
| **1.1** | **ELIMU SEKONDARI** | | | | | |
| 1.1.1 | Ujenzi wa vyumba 11 vya madarasa na Ofisi 5 katika katika Shule ya Sekondari Kakonko | - | 220,000,000.00 | 208,886,164.50 | 94.95 | Chumba 1 cha darasa na Ofisi 1 ujenzi upo hatua ya kuweka sakafun na 10 na ofisi 5 ujenzi upo hatua ya kuskimu ukuta na dari. |
| 1.1.2 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 2 katika Shule ya Sekondari Kanyonza | - | 60,000,000.00 | 37,855,900.00 | 63.09 | Vyumba 2 vya madarasa na ofisi 1 kechi na plasta tayari zinasubiriwa bati ili kuezeka. Aidha chumba 1 cha darasa na ofisi 1 utekelezaji umekamilika kwa kiasi kikubwa imebaki kufunga milango. |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.1.3 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa na Ofisi 2 katika katika Shule ya Sekondari Buyungu | - | 80,000,000.00 | 57,364,199.40 | 71.71 | Ujenzi wa vyumba 4 na ofisi 2 majengo yameezekwa na kupigwa plasta ndani, kazi ya kufunga gypsum inaendelea |
| 1.1.4 | Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa na Ofisi 3 katika Shule ya Sekondari Kasanda | - | 120,000,000.00 | 88,635,100.00 | 73.86 | Vyumba 6 vya madarasa na ofisi 3 ujenzi upo hatua ya kufunga gypsum. |
| 1.1.5 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 Shule ya Sekondari Mugunzu | - | 40,000,000.00 | 36,531,500.00 | 91.33 | Ujenzi wa vyumba 2 na ofisi 1 jengo limeezekwa na kupigwa plasta ndani, kazi ya kujenga hanamu inaendelea |
| 1.1.6 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 katika Shule ya Sekondari Gwanumpu | - | 60,000,000.00 | 29,810,000.00 | 49.68 | Ujenzi wa vyumba 3 na ofisi 1 jengo limeezekwa, kupigwa plasta na kazi kujenga hanamu za ndani na kunyoosha kopla inaendelea |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.1.7 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 katika Shule ya Sekondari Rugenge | - | 60,000,000.00 | 48,862,300.00 | 81.44 | Ujenzi wa vyumba 3 na ofisi 1 upo hatua ya kufunga gypsum board, utengenezaji wa viti na meza unaendelea. |
| 1.1.8 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 katika Shule ya Sekondari Shuhudia | - | 60,000,000.00 | 43,264,800.00 | 72.11 | Ujenzi wa vyumba 3 na ofisi 1 upo hatua ya kusuka mbao za blundering. Utengenezaji wa viti na meza unaendelea. |
| 1.1.9 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 katika Shule ya Sekondari Ndalichako | - | 60,000,000.00 | 39,135,000.00 | 65.23 | Ujenzi wa vyumba 3 na ofisi 1 upo hatua ya kupiga plasta. Utengenezaji wa viti na meza unaendelea. |
| 1.1.10 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa na Ofisi 2 katika Shule ya Sekondari Muhange | - | 80,000,000.00 | 75,156,100.00 | 93.95 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi 2 upo hatua ya kufanya skiming ya ukuta kwa ajili ya kupaka rangi. Utengenezaji wa viti na meza unaendelea |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.1.11 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 katika Shule ya Sekondari Kashoza | - | 40,000,000.00 | 31,637,765.00 | 79.09 | Ujenzi wa vyumba 2 na ofisi 2 ujenzi upo hatua ya kufunga gypsum. Utengenezaji wa viti na meza unaendelea |
| 1.1.12 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 katika Shule ya Sekondari Nyamtukuza | - | 40,000,000.00 | 36,091,735.00 | 90.23 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi 1 upo hatua ya kufunga gypsum na kuweka sakafu. Utengenezaji wa viti na meza unaendelea |
| | **Jumla Ndogo** | | **920,000,000.00** | **733,230,563.90** | | |
| **1.2** | **ELIMU MSINGI** | | | | | |
| 1.2.1 | Ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Itumbiko | | 80,000,000.00 | 51,111,997.00 | 63.89 | Ujenzi wa bweni upo hatua ya kenchi pamoja na kutungilia. |
| | **Jumla Ndogo** | | **80,000,000.00** | **51,111,997.00** | | |
| **1.3** | **Afya** | | | | | |
| 1.3.1 | Ujenzi wa jengo la huduma za dharura (Emergency Medical Department - EMD) | - | 300,000,000.00 | - | - | Fedha hizi pamoja na ramani ya ujenzi zilichelwa kupokelewa tofauti na za madarasa na Halmashauri inaendelea na taratibu |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | za manunuzi. |
| | Ujenzi wa nyumba ya watumishi wa afya yenye uwezo wa kubeba familia familia tatu | - | 90,000,000.00 | - | - | Fedha hizi pamoja na ramani ya ujenzi zilichelwa kupokelewa tofauti na za madarasa na Halmashauri inaendelea na taratibu za manunuzi. |
| | **Jumla** | - | **390,000,000.00** | - | - | |
| | **JUMLA YA FEDHA ILIYOPOKELEWA NJE YA BAJETI** | | **1,390,000,000.00** | **784,342,560.90** | **56.43** | |

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walijadili kama ifuatavyo;

- **Kuhusu hatua iliyofikiwa katika ujenzi**

Mhandisi wa ujenzi alieleza shule nyingi zipo katika upauaji na plasta hivyo zinaenda vizuri. Mwenyekiti alihoji kuhusu shule ya Sekondari Ndalichako. Mhandisi wa Ujenzi alieleza shule hiyo ilikuwa nyuma lakini wanaendelea vizuri.

**Taarifa ilipokelewa.**

**MUHT.NA.5/CMT/2021/22/8. UJENZI WA MIRADI INAYOTEKELEZWA KWA MAPATO YA NDANI.**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa kisha wajumbe kujadili kama ifuatavyo;

- **Kuhusu mgawanyo wa fedha kwa Zahanati na hatua iliyofikiwa**

Mganga Mkuu alieleza Zahanati ya Kihomoka ipo hatua ya jamvi. Mwenyekiti alieleza milioni 30 zimepelekwa Kihomoka na Njoomlole na milioni 20 pia zimepelekwa kwenye Zahanati.

**Taarifa ilipokelewa.**

**MUHT.NA.5/CMT/2021/22/9.MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

- **Kuhusu Ujenzi wa stendi**

Mwenyekiti alielekeza Mhandisi wa Ujenzi awasiliane na Mkandarasi mshauri na mkandarasi ili wakutane site na kufanya kikao.

- **Kuhusu ujenzi wa hospitali ya Wilaya**

Mhandisi afuatilie mafundi ili wafunge milango.

- **Kuhusu kuvunja mkataba na TBA, kufanya marekebisho ya vyumba pamoja na ujenzi wa 'wing' yenye kenchi juu.**

Afisa Mipango alieleza taratibu za kuandaa mikataba zinaendelea. Mwenyekiti alisisitiza mkataba uwasilishwe kwake Alhamisi tarehe 16 Desemba 2021 ili kusaini. Mwenyekiti aliagiza fundi afuatiliwe ili kutengeneza 'wing, ambayo ina kenchi juu. Mweka Hazina aliagizwa kufuatilia hilo. Aidha marekebisho ya vyumba yafanyike ili idara moja iwe na vyumba vya pamoja na chumba cha mkuu wa idara na choo chake.

- **Kuhusu Machinjio ya Kasanda na ujenzi wa machinjio mpya Kakonko mjini**

Afisa Mifugo alieleza walipitia azimio ni kukubaliana kutengeneza jengo lenye mfumo wa maji taka na shimo kwa mawe kwa gharama ya Tshs.9,822,900/=. Mwenyekiti alimwagiza Afisa Mifugo kupitia upya gharama hizo na kuangalia uwezekano wa kuingiza marekebisho kwenye bajeti. Aidha Afisa Ardhi atafute eneo mjini kwa ajili ya ujenzi wa machinjio mpya na ya kisasa. Mweka Hazina alishauri kujenga kisahani cha machinjio badala ya kujenga jengo jipya Kasanda. Alishauri kibanda kilichopo kiboreshwe wajumbe walishauri kipaumbele kiwe kujenga machinjio Kakonko mjini kwani ndio Wilayani. Menejimenti iliazimia suala hili lifanyiwe kazi kabla ya kikao cha kamati ya fedha. Mwenyekiti alisisitiza suala la machinjio liandaliwe andiko kupitia mradi wa mazingira ili kujenga machinjio mapya.

- **Kuhusu Vibanda soko kuu**

Afisa biashara aliwasilisha muhtasari wa kikao cha menejimenti na wamiliki wa vibanda wa tarehe 01.12.2021. Baada ya kusoma muhtasari huo Mwenyekiti alisisitiza msimamo wa Halmashauri ni ule ule wa kujenga vibanda vya kisasa. Aliagiza taarifa hiyo kuwasilishwa katika kikao cha kamati ya fedha tarehe 16.12.2021.

- **Kuhusu Mnada wa mifugo kihomoka.**

Afisa mifugo alieleza walikwenda Kihomoka na kukubaliana kuwa mnada ufanyike mara 02 kwa mwezi yaani Jumatatu ya kwanza na ya tatu ya mwezi . Mwenyekiti alisisitiza miti isiondolewe kwenye eneo la mnada bali matawi yapunguzwe. Aidha timu inayotakiwa kwenda Kihomoka iende siku ya Jumanne tarehe 14/12/2021 ili kukamilisha hilo.

- **Kuhusu Wakusanya mapato**

Mweka hazina alieleza siku hiyo ilikuwa ni siku ya kusaini mikataba mipya na wakusanya mapato ambapo mkataba ni mwaka mmoja lakini utakuwa wa miezi 3 hivyo mikataba hiyo imesainiwa na wahusika watapangiwa vituo vipya.

- **Kuhusu Maombi ya idhini ya kufungua akaunti za 'Imprest' katika benki ya CRDB.**

Mweka hazina aliwasilisha taarifa na kueleza kuwa sababu ya kufungua akaunti benki ya CRDB ni kurahisisha utoaji wa huduma za malipo kwa wakati, kuwezesha kulipa kwa haraka wateja waliofungua akaunti benki ya CRDB, kuomba huduma za malipo na kuongeza kasi za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kuwa itaondoa urasimu katika benki inayotumika. Hoja iliungwa mkono.

**MUHT.NA.5/CMT/2021/22/10.KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na kufunga kikao saa 12:15 jioni.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ...Ndalli... | ...Hafaya: 13/12/2021. |
| **MWENYEKITI** | **TAREHE** |
| ...Hafaya:... | ...13/12/2021... |
| **KATIBU** | **TAREHE** |